# KONGAMANO LA 4 LA KIMATAIFA KUHUSU AFYA YA UMMA BARANI AFRIKA

**26–29 NOVEMBA 2024 • RABAT, MOROKO**

International CPHIA 2024
Conference on Public Health in Africa

**KUELEKEA KUJITEGEMEA ILI KUFIKIA HUDUMA YA AFYA KWA WOTE NA USALAMA WA AFYA BARANI AFRIKA**

## Muhtasari wa Wasilisho la Maonyesho ya CPHIA 2024

### Kuhusu CPHIA

Kongamano la kila mwaka la Afya ya Umma barani Africa (CPHIA), mradi wa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa barani Afrika (Africa CDC), unatoa mfumo wa kipekee unaongozwa na Waafrika kwa viongozi na wanasayansi kote barani kushiriki taarifa za maendeleo ya kisayansi, mafunzo tuliyojifunza katika utoaji wa huduma bora za afya, na suluhu bunifu za afya ya umma zenye msingi wa ushahidi ili kushughulikia changamoto za kiafya katika Afrika.

CPHIA 2024 litaandaliwa mjini Rabat, Moroko, kuanzia tarehe 26 hadi 29 Novemba 2024, huku likitarajiwa kushirikisha hadi viongozi 10,000 wa kisiasa, watunga sera za afya, wabunifu na watetezi wa afya, wajasiriamali, wanasayansi watafiti, wataalamu wa afya, wawakilishi wa raia na vijana. Tukio hili, linaloandaliwa kwa pamoja na Africa CDC na Wizara ya Afya na Ulinzi wa Jamii ya Ufalme wa Moroko, litaangazia maendeleo ya Afrika kwenye jukwaa la kimataifa chini ya mada "Kuelekea katika Kujitegemea ili Kufikia Huduma ya Afya kwa Wote na Usalama wa Afya Barani Afrika" na linaangazia nyanja nane za mada.

Hili litakuwa kongamano la nne, la kwanza lilifanyika mwanzoni kwa njia ya mtandao mwaka wa 2021 na kisha la pili na tatu ana kwa ana mnamo mwaka wa 2022 na 2023 huko Kigali, Rwanda, na Lusaka, Zambia, mtawalia. Huku nchi za Afrika zikiharakisha ufanikishaji wa huduma ya afya kwa wote, CPHIA za kila mwaka zinasaidia kubaini jinsi Afrika inaweza kujitegemea zaidi katika utoaji wa huduma bora za afya ili kufikia Afrika yenye afya, ustawi zaidi – kwa bara, na ulimwengu.

### Maombi ya Maonyesho

CPHIA 2023 ilijumuisha nafasi ya maonyesho yenye nguvu na umahiri. Mwaka huu, tunalenga kukuza hali hii hata zaidi. Tunafurahi kuwapa waonyeshaji fursa nyingine ya kuonyesha teknolojia, suluhu na huduma zao za kisasa kwa hadhira tofauti ya wataalamu wa tasnia, wawekezaji, watunga sera na magwiji. Maonyesho yetu ya 2024 yanakusudia kuwa ya kuvutia, bunifu na yenye kuleta mabadiliko, yakijumuisha vipengele vipya na mwingiliano ulioimarishwa.

Tunakaribisha maombi kutoka kwa mashirika katika sekta zote zilizojitolea kuunganisha viongozi wa afya ya umma, kukuza ushirikiano, na kutengeneza mkondo mpya wa afya barani Afrika.
Waandaaji wa maonyesho wanatarajiwa kutangaza zaidi kongamano kupitia mitandao yao na kuhudhuria CPHIA 2024 mjini Rabat mnamo Novemba 2024.

AfricaCDC
Centres for Disease Control and Prevention

**Limeandaliwa na:**

Ministère de la Santé et de la Protection Sociale

Maonyesho haya yatawekwa kufikia tarehe 25 Novemba na kubaki hadi tamati ya mkutano tarehe 29 Novemba. Angalia hapa chini kwa mwongozo na maelezo kuhusu jinsi ya kuwasilisha ombi la maonyesho. Tafadhali kumbuka kuwa maelezo yote ya maonyesho yatathibitishwa baada ya pendekezo kuidhinishwa.

**Wito huu utafungwa tarehe 23 Septemba 2024. Tafadhali jaza na uwasilishe fomu inayohitajika ya ombi kufikia saa 23:59 EAT/20:59 UTC.**

**Waandaaji wataarifiwa kuhusu hali ya pendekezo lao kufikia tarehe 11 Oktoba 2024.**

## Miongozo ya Kutuma Maombi

Ombi lako la kuandaa maonyesho lazima lijumuishe yafuatayo:

- Kichwa kinachopendekezwa cha maonyesho.
- Maelezo ya maonyesho yanayopendekezwa na jinsi yanavyoendana na maono ya Africa CDC kwa bara la Afrika lililo salama, lenye afya na mafanikio (maneno 250 au chini).
- Lengo kuu la maonyesho, kama vile mwonekano/kukuza chapa, uwasilishaji wa bidhaa, utetezi au uchangishaji fedha, n.k. (maneno 100 au chini).

Tunahimiza dhana bunifu na za kipekee katika uwekaji wa maonyesho.

Ikiwa vifurushi vifuatavyo havikidhi mahitaji ya pendekezo lako la maonyesho, tafadhali taja hili katika ombi lako; mapendekezo maalum nje ya chaguo za vifurushi yatazingatiwa kulingana na hali.

## Vifurushi vya Maonyesho

***Uthabiti wa Shaba (Bronze Resilience):*** **25,000MAD/2,500USD** *(Kwa mashirika yasiyo ya kibiashara kutoka Afrika)*

- Nembo kwenye ukuta wa maonyesho wa CPHIA 2024
- Usajili wa bure wa kongamano kwa watu wawili

***Shaba iliyoongezwa (Bronze plus):*** **100,000MAD/10,000USD** *(Kwa mashirika ya kimataifa yasiyo ya kibiashara)*

- Nembo kwenye ukuta wa maonyesho wa CPHIA 2024
- Usajili wa bure wa kongamano kwa watu wawili
- Ujumuishaji wa kipeperushi kwenye mkoba wa kuwakaribisha wahudhuriaji wa kongamano

***Muungano (Union)*****: 100,000MAD/10,000USD** *(Kwa taasisi za serikali, taasisi za kimasomo na utafiti za Afrika pekee)*

- Nembo kwenye ukuta wa maonyesho wa CPHIA 2024
- Usajili wa bure wa kongamano kwa watu wawili
- Ujumuishaji wa kipeperushi kwenye mkoba wa kuwakaribisha wahudhuriaji wa kongamano

**Fedha ya Amani (Peace Silver): 300,000MAD/30,000USD** *(Kimefunguliwa kwa mashirika yote ya Afrika na ya kimataifa yasiyo ya kibiashara, taasisi za kimasomo na utafiti na vyama vya ushirika).*

- Kibanda cha kawaida (mita 2.5 kwa mita 3)

- Nembo kwenye ukuta wa maonyesho wa CPHIA 2024
- Usajili wa bure wa kongamano kwa watu wawili
- Beji mbili za waonyeshaji kwa wageni
- Tiketi mbili kwa tamasha la jioni
- Punguzo la asilimia 50 kwa kuandaa tukio la kando/ndogo
- Ujumuishaji wa brosha ya kampuni (kurasa 2) kwenye mkoba wa wajumbe na waonyeshaji
- Ujumuishaji wa bidhaa ya utangazaji kwenye mkoba wa wajumbe

**Dhahabu ya Ubuntu (Ubuntu Gold): 500,000MAD/50,000USD** *(Kimefunguliwa kwa mashirika yote ya Afrika na ya kimataifa yasiyo ya kibiashara, taasisi za kimasomo na utafiti na vyama vya ushirika).*

- Kibanda cha ukubwa wa wastani (mita 3.5 kwa mita 4)
- Uwekaji wa nembo mahali maalum
- Usajili wa bure wa kongamano kwa watu watatu
- Pasi ya VIP (inaruhusu kuketi sehemu ya VIP wakati wa vikao vya ufunguzi, mkutano na kufunga)
- Beji tatu za waonyeshaji kwa wageni
- Tiketi tatu kwa tamasha la jioni
- Tukio moja lisilolipishwa la kando
- Ufadhili kwa watafiti chipukizi
- Ujumuishaji wa bidhaa ya utangazaji kwenye mkoba wa wajumbe
- Video ya utangazaji ya kampuni katika nafasi za mikutano
- Ujumuishaji wa brosha ya kampuni (isizidi kurasa 4) kwenye mkoba wa wajumbe na waonyeshaji

**Platinamu ya Uhuru (Uhuru Platinum): 750,000 MAD/75,000USD** *(Kimefunguliwa kwa mashirika yote ya Afrika na ya kimataifa yasiyo ya kibiashara, taasisi za kimasomo na utafiti na vyama vya ushirika).*

- Kibanda kikubwa (mita 4.5 kwa mita 5)
- Uwekaji wa nembo mahali maalum
- Usajili wa bure wa kongamano kwa watu watano
- Pasi mbili za VIP (Zinaruhusu kuketi sehemu ya VIP wakati wa vikao vya ufunguzi, mkutano na kufunga)
- Beji nne za waonyeshaji kwa wageni
- Tiketi nne kwa tamasha la jioni
- Tukio moja lisilolipishwa la kando
- Chumba maalum cha mkutano
- Ufadhili kwa watafiti chipukizi
- Ujumuishaji wa brosha ya kampuni (isizidi kurasa 4) katika mkoba wa wajumbe
- Ujumuishaji wa bidhaa ya utangazaji kwenye mkoba wa wajumbe
- Ujumuishaji wa nembo ya kampuni kwenye tovuti ya mkutano, programu ya mwisho na mwongozo wa mkutano.

Kwa maelezo zaidi kuhusu kongamano la CPHIA 2024, tembelea [www.CPHIA2024.com](http://www.CPHIA2024.com). Kwa maswali kuhusu maonyesho, tuma barua pepe kwa: CPHIAexhibitions@africacdc.org